

The
Management
University
of Africa



Sponsored by the Kenya Institute of Management

UNDERGRADUATE UNIVERSITY EXAMINATIONS

SCHOOL OF MANAGEMENT AND LEADERSHIP

DEGREE OF BACHELOR OF EDUCATION ARTS

KIS 426: ISIMU JAMII

TAREHE: 30 MACHI 2026

MUDA: MASAA MAWILI

JUMLA YA ALAMA: 70

MAAGIZO:

1. Andika nambari yako ya usajili katika kitabu cha majibu ulichopewa.
2. **USIANDIKE CHOCHOTE** kwenye karatasi ya maswali
3. Karatasi hii ya mtihani ina maswali **sita (6)**
4. **SWALI LA KWANZA** ni la lazima
5. Jibu maswali mengine **MATATU** kutoka sehemu zilizobaki.
6. **SWALI LA KWANZA** lina alama **25** ilhali maswali mengine yana **ALAMA 15** kila moja.
7. **Jibu majibu yako yote katika kitabu cha majibu/ mtihani ulichopewa.**

SWALI LA KWANZA

- a) Kwa kutolea mifano mwafaka, onyesha uhusiano uliopo baina ya Isimujamii na taaluma zifuatazo
- i) Anthropolojia (alama 3)
 - ii) Sosholojia (alama 3)
 - iii) Jiografia (alama 3)
- b) Eleza uhusiano uliopo baina ya lugha na jamii, (alama 6)
- c) Jadili matatizo yanayokumba maenezi ya Kiswahili nchini Kenya sasa na ueleze juhudi zinazopaswa kuchukuliwa ili kuyatatua. (alama 10)

SWALI LA PILI

- a) Eleza maana ya usanifishaji wa lugha (alama 3)
- b) Changanua wajibu wa lugha ya Kiswahili kama lugha ya Kimataifa. (alama 12)

SWALI LA TATU

- a) Upangaji lugha ni nini? (alama 2)
- b) Jadili mchakato wa upangaji lugha. (alama 8)
- c) Eleza majukumu Matano ya upangaji lugha. (alama 5)

SWALI LA NNE

- a) Lahaja ni nini? (alama 2)
- b) Huku ukitolea mifano, jadili aina mbili kuu za lahaja. (alama 6)
- c) Fafanua mambo ambayo huchangia kuzuka kwa lahaja. (alama 7)

SWALI LA TANO

- a) Jadili mchango wa Nadharia ya Sapir Whorf katika kuangazia matumizi ya lugha katika jamii. **(alama 7)**
- b) Fafanua hatua nane ambazo zinaweza kuchukuliwa na serikali kuzifufua lugha za kwanza ambazo zinaendelea kudidimia kimatumizi. **(alama 8)**

SWALI LA SITA

- a) Kwa kutolea mifano mwafaka, tofautisha kati ya Pijini na Krioli. **(alama 8)**
- b) Jadili sababu mbali mbali zinazoweza kusababisha kufa au kufifia kwa lugha. **(alama 7)**